JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Mkuu wa shule
0753161461/0623673740 Makamu mkuu wa shule 0768310624
Matron 0756025091 / 0758083877

Shule ya sekondari Kasangezi
S.L.P 315
Kasulu Tarehe

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KASANGEZI HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU MKOA WA KIGOMA MWAKA 2022

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022. Shule ya sekondari kasangezi ipo umbali wa kilometa 27 kusini mwa mji wa Kasulu . usafiri wa daladala / basi kutoka mjini Kasulu unapatikana katika kituo cha daladala / mabasi makaburini / stendi mpya kwa nauli ya shilingi elfu tatu 3000/=.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe ..... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ....., na mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia :**

2.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule ni sketi (2) za dark blue (kitambaa kizito) na shati mbili nyeupe mikono mifupi kwa wasichana na suruali (2) za dark blue(kitambaa kizito) na shati mbili nyeupe mikono mifupi kwa wavulana Mshono ni wa kawaida kwa wavulana, suruali isiwe ya kubana (modo) na iwe na mkunjo wa chini (turn up), kwa wasichana sketi inatakiwa ifike kwenye jicho la mguu (juu kidogo ya unyayo) mshono ni linda boksi. Siyo jukumu la shule kushona sare za wanafunzi ILA wazazi watakaopenda kushona sare hizo shuleni wataelekezwa sehemu ya kupata sare hizo kwa bei nafuu kwa gharama zifuatazo:(sketi 2 @16000 = Tsh.32000, suruali 2 @14000 =Tsh.28000).

b) Rangi ya hijab kwa anaye hitaji ifanane na kitambaa cha shati (nyeupe) na ifike kwenye viganja vya mikono.

c) Sare ya michezo kwa shule ni jezi za blue ya Chelsea ziwe mbili (t shirt za bluu mikono mifupi na truck suit ya bluu yenye mistari myeupe pembeni kwa wasichana na kwa wavulana. Ziwe kuanzia pair 2).

d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, Soksi jozi mbili nyeusi

e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.

f) Sweta la rangi ya dark blue, mikono mirefu isiwe na mistari wala maandishi yoyote

g) Nguo za kushindia (shamba dress). Wanafunzi waje na Nguo hizo , kwa wale wazazi watakaopenda wanafunzi washonewe karibu na shule wataelekezwa mahali pa kuzipata kwa gharama nafuu, kwa mchanganuo ufuatao:-

   i. Kwa wasichana ni gauni 2(mbili) za rangi ya damu ya mzee. Zinapatikana shuleni kwa gharama ya @20000 =Tsh.40000, Pia Kwa wavulana ni suruali mbili (2) rangi ya damu ya

mzee zinapatikana shuleni kwa gharama ya @14000 =Tsh.28000 .

ii. Tshirt za shule zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh.10000/=

NB.

- ✔ Mwanafunzi hatakiwi kufika shuleni na **NGUO ZA NYUMBANI** (vaa uniform au truck suit),
- ✔ SIMU hazitakiwi Kabisa hapa shuleni **(USIJE NA SIMU).**

2.2 **Ada na michango ya shule**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000 unaweza kulipa shilingi 35,000 kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunt ya shule iitwayo KASANGEZI SECONDARY SCHOOL CAPITATION .A/C NUMBER 51401200147 katika benki ya NMB (tafadhari andika jina la mwanafunzi na kidato kwenye pay in slip)

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni :

i. Shilingi 20000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

ii. Shillingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha

iii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima (mock)

iv. Fedha ya tahadhari 10000/=itatolewa kila mwaka. (haitarejeshwa)

v. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya Huduma ya kwanza na Bima ya afya (CHF) . itatolewa kila mwaka. **Tshs 5,000/= (kwa wale ambao tayari wameshajiunga na bima mfano. NHIF n.k)**

vi. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

vii. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.

viii. Shilingi 2,000/= nembo ya shule.

Jumla ya ada na michango kwa mwaka ni shilingi **188,000/=**

NB. MICHANGO YOTE PAMOJA NA ADA VIWEKWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE.

JINA LA AKAUNTI : KASANGEZI SECONDARY SCHOOL CAPITATION.

AKAUNTI NAMBA : 51401200147

BANK: NMB BANK.

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni :

i. Jembe 1 lenye mpini, mfagio wa nje.

ii. Mopper , Hard bloom (mfyagio mgumu),

iii. (slesha) au panga

iv. Hand brush (brashi ya kusugulia vyoo)

v. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko

vi. Ream za karatasi 1 kila mwaka (plain paper nyeupe Double A, A4)

vii. Rolled paper 1 yenye mistari. kila mwaka

Mahitaji mengineyo binafsi kwa mwanafunzi ni;

i. Scientific calculator kwa wale wanaosoma geography.

ii. Godoro 2.5X 6

iii. Mashuka pair 2 pink kwa wasichana na foronya 1 yenye rangi ya shuka

iv. Mashuka pair 2 blue kwa wavulana na foronya 1 yenye rangi ya shuka

v. Blanket 1 rangi yeyote na chandarua rangi ya bluu kwa wote

vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko, na kikombe)

vii. Tochi kwa matumizi binafsi .

viii. Daftari 9

ix. Oxford dictionary/ kamusi ya kiswahili.

x. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika kama ifuatavyo (kwa matumizi binafsi)

A. GEOGRAPHY

i. Human and economical geography advanced level paper 2 by D.T Msabila

ii. Practical geography A-level for high schools and colleges by Zist Kamili

iii. Physical geography By D.T Msabila

iv. Principle of physical geography by Monk House F.J

v. A study in physical geography for advanced students by Pritchard J.M

vi. Physical and human geography by Ojany

B. KISWAHILI

i. Nadharia ya lugha ya Kiswahili :1

ii. Samikisa na samakisa

iii. Nadharia ya fasihi kidato cha 5&6

C. HISTORY

i. Contemporary historical events by Mwl. Shibitali CK.Tumaini

ii. Mastering history paper 1 by Kato

D. ENGLISH

Advanced level; A practical Approach second edit on by N.Asheli

E. GENERAL STUDIES

F. KWA WANAFUNZI WA MASOMO YA SCIENCE MNASHAURIWA KUNUNUA VIFAA VIFUATAVYO.

SCIENTIFIC CALCULATOR, DISSECTION KIT, DISSCECTION TRAY NA LAB COAT.

3. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa siku 90 bila taarifa / utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usio kubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele
vii. fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi ulio kubalika na uongozi wa shule .
viii. Kufuga ndevu
ix. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
x. Uvutaji wa sigara.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiii. Kutembelea majumba ya starehe nyumba za kulala wageni
xiv. KUMILIKI, KUKUTWA AU KUTUMIA SIMU YA MKONONI KATIKA MAZINGIRA YA SHULE.
xv. Kudharau bendera ya taifa
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatanisho na Fomu muhimu

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika mgomo , fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya mzazi kukiri kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule .

d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA

CHARLES LUGENDA

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU SHULE YA SEKONDARI KASANGEZI

FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

A. **Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi**

1. Jina kamili la mwanafunzi……

2. Mahali anapoishi Kijiji/ mtaa…… Mkoa …… wilaya ……

3. Tarehe ya kuzaliwa ……. Kijiji alichozaliwa …….. kabila……..

4. Shule ya sekondari (''O'' level) aliyosomea……

Habari za wazazi / walezi

1. Jina kamili la baba /mlezi……

2. Jina kamili la mama / mlezi……

3. Kazi ya baba / mlezi……..... ……

Kazi ya mama / mlezi……

4. Je baba yupo hai. Ndiyo/ hapana.

5. Je mama yupo hai . ndiyo /hapana.

Kukitokea dharura ndugu wengine wanaoweza kujulishwa ni:-

1. Jina kamili ……. uhusiano uliopo… ..... namba ya simu…..……..

2. Jina kamili……Uhusiano uliopo… ..... namba ya simu……..

Mimi ..... niliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari kasangezi kidato cha tano(5) mwaka 2022.

Mimi ..... Nathibitisha kuwa taarifa hizo ni sahihi na za kweli

Jina kamili la mzazi / mlezi……Saini……Simu……..

B. **Mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.**

1. Naahidi kutii na kutekeleza masharti na maelekezo mbalimbali ya shule chini ya uongozi wa shule. Sitashiriki katika migomo, fujo na makosa yoyote ya jinai

2. Kama mwanafunzi naahidi kuwa mtiifu na mnyenyekevu mahali popote kwa kuzingatia kanuni,taratibu na sheria za shule hii

3. Endapo nitakiuka kanuni,taratibu na sheria za shule hii nastahili kuadhibiwa kulingana na

itakavyoelekezwa na kuamriwa na mwalimu, mkuu wa shule na bodi ya shule kwa ajili ya kurekebisha mwenendo wangu, kuleta heshima ya shule, kuleta amani na utulivu shuleni na kuendeleza malezi bora kwa vijana wa Tanzania

4. Nathibitisha kuwa nimesoma kwa makini na matamko haya nayatoa kwa ajili yangu mwenyewe .

Jina la mwanafunzi…… Saini …….. tarehe ……

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU SHULE YA SEKONDARI KASANGEZI

Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

1. Mimi ..... mzazi/mlezi wa mwanafunzi ..... aliyechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari kasangezi mwaka 2022.
2. Nakubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kwani natambua kuwa malezi bora ya mtoto ni matunda kati ya walimu na wazazi/ walezi
3. Aidha natambua kuwa nidhamu ina mchango mkubwa katika maendeleo mazuri ya kitaaluma ya mwanafunzi.
4. Aidha natambua kuwa nidhamu ina mchango mkubwa katika maendeleo mazuri ya kitaaluma ya mwanafunzi.

Jina kamili la mzazi/ mlezi ……

Namba ya simu ……

Saini ……

Tarehe……

PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KASANGEZI SECONDARY SCHOOL

Stool examination……

Urinalysis …….

Blood count (white and white) ……

Syphilis test……

T.B Test ……

Eye test……
Spleen……

Additional information e.g physical defect impairment(s) , chronic infections or family disease
……
……
……
……

I certify that I have examined above student and recommended that he/ she fit /unfit to pursue further

education .

MEDICAL EXAMINATION FORM (To be completed by a medical of cer in respect of all form five (V) entrance)

Student's full name ……..

Age ……(years)……..

Sex…….